**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 1 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i1.1038
*Utata wa Baadhi ya Viambishi Tamati katika Vitenzi vya Kiswahili*

# Utata wa Baadhi ya Viambishi Tamati katika Vitenzi vya Kiswahili

**Issaya Lupogo**
*Chuo Kikuu Mzumbe, Tanzania* na *Chuo Kikuu cha Pretoria, Afrika Kusini*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Kupokelewa: 2025-01-12*
*Kurekebishwa: 2025-04-29*
*Kukubaliwa: 2025-05-05*
*Kuchapishwa: 2025-05-06*

***Maneno Muhimu***
Kiswahili
Viambishi
Viambishi Tamati Ishilizi
Vitenzi

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Lupogo, I. (2025). Utata wa Baadhi ya Viambishi Tamati katika Vitenzi vya Kiswahili. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(1), 47-58.

*Copyright © 2025*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Baadhi ya viambishi tamati katika vitenzi vya Kiswahili vimechanganuliwa na kuelezwa kwa namna zinazokinzana miongoni mwa wanaisimu mbalimbali. Makala hii inafafanua utata unaojitokeza katika suala hilo na kisha kupendekeza suluhisho muafaka. Makala hii ni matokeo ya utafiti wa mapitio ya machapisho pamoja tajiriba ya elimu ya sayansi ya lugha ya Kiswahili ya mwandishi akiwa na uzoefu wa kufundisha isimu ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza chuoni kwa miaka zaidi ya kumi. Aidha, mwandishi anajenga hoja za kimantiki baada ya tafakari tunduizi ya masuala tatanishi huku hoja hizo zikishadadiwa kwa kupanua data husika. Upanuzi wa baadhi ya data ulisaidiwa na wadau wa Kiswahili katika makundi ya *WhatsApp ya Kiswahili* na isimu. Utata wa ufafanuzi na uchanganuzi unaooneshwa katika makala hii unahusu baadhi ya viambishi tamati ishilizi "*a, e, i* na *u*,'' katika vitenzi vya Kiswahili. Halikadhalika, utata mwingine ni kuhusu viambishi tamati vilivyopata kuchanganuliwa au kubainishwa na wanaisimu waliotangulia. Baadhi ya wanaisimu wamechanganua kwa namna hii: "*-eni*/*-uni/-ini*" (mf. lim-*eni*/thubut-*uni*/safir-*ini*) huku wanaisimu wengine wakichanganua hivi: "*-ni*" (mf. lime-*ni*/thubutu-*ni*/safiri-*ni*). Makala hii imependekeza uchanganuzi na ufafanuzi mpya wa viambishi hivyo: "*-en-i*" (mf. lim-*en-i*), "-*un-i*" (mf. thubut-*un-i*) na "*in-i*" (mf. safir-*in-i*). Katika uchanganuzi huu mpya, viambishi *-en-*, *-un-*, na *-in-* vinarejelea dhana ya upamoja.

## Utangulizi

Makala hii inapendekeza suluhisho la mkanganyiko wa uchanganuzi na ufafanuzi wa baadhi ya viambishi tamati katika vitenzi vya Kiswahili. Kitenzi ni mojawapo ya aina za maneno ambayo ipo katika kila aina za maneno zilizowahi kutolewa na wanaisimu mbalimbali. Kwa mfano, Kihore na wenzake (2003) wamefafanua aina saba za maneno: nomino, vitenzi, viwakilishi, viunganishi, vielezi, vivumishi na viingizi. Wakati Taasisi ya Taaluma za Kiswahili-TATAKI (2004) katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu wana aina nane: nomino, vitenzi, viwakilishi, viunganishi, vielezi, vivumishi, vihusishi na vihisishi. Kitenzi ni aina ya neno linalotaja ufanyikaji wa tendo au jambo. Mfano: Juma analima, neno "analima" ni kitenzi. Vitenzi vya Kiswahili hujengwa na viambishi na mzizi.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2012), viambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno pamoja na mofimu hizo. Mzizi unafafanuliwa na Rubanza (1996) kuwa ni sehemu ya neno ambayo huwa haibadiliki. Kuna viambishi vya namna mbili katika Kiswahili: viambishi awali na viambishi tamati.

Massamba na wenzake (2012) wamefafanua viambishi awali kuwa ni vile viambishi vinavyojitokeza mwanzoni mwa mzizi wakati viambishi tamati ni vile viambishi vinavyojitokeza mwishoni mwa mzizi wa neno.

Makala hii inaangazia baadhi ya viambishi tamati katika vitenzi vya Kiswahili. Lengo likiwa kutafuta ufumbuzi wa mkanganyiko wa uchanganuzi na ufafanuzi wa irabu zinazojitokeza mwishoni mwa vitenzi vya Kiswahili ambazo ni *a, e, i* na *u*. Pia, makala hii inachunguza maumbo kdhaa yaliyopata kuchanganuliwa na wanaisimu waliotangulia: *-eni/-uni/-ini* na *-ni* kama katika maneno *nendeni*, *thubutuni* na *safirini.* Hii ina maana kwamba wapo wanaisimu wanaochanganua neno nendeni hivi: nend-eni, na wapo wanaochananua neno hilohilo hivi: nende-ni. Aidha, kuhusu viambishi tamati ishilizi *a, e, i,* na *u;* wanaisimu mbalimbali wanakinzana katika kueleza dhima za viambishi hivyo. Pamoja na kubainisha mikanganyiko ya kiuchanganuzi iliyopo katika maeneo tajwa, makala hii inatoa mapendekezo ya utatanisho huo.

**Methodolojia**

Matokeo ya makala hii yanatokana na kufanya mapitio ya maandiko mbalimbali maktabani kama yanavyojitokeza katika sehemu ya marejeleo, na kisha kujenga hoja zenye mantiki. Suala hilo limewezakana kwa kuwa mwandishi ana tajiriba inayotokana na uzoefu wake wa kufundisha isimu ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza chuoni kwa miaka zaidi ya kumi. Aidha, hoja hizo zinashashadiwa kimantiki kwa kupanua data husika. Upanuzi wa baadhi ya data ulisaidiwa na wadau wa Kiswahili katika makundi mbalimbali ya *WhatsApp* ya Kiswahili na Isimu: Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani (CHAUKIDU), Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA), Koja la Walumbi wa Kiswahili, na *Linguistic Circle*. Hivyo, hoja mpya zinazojengwa katika makala hii ni kutokana na tafakari tunduizi ya kimantiki ya mwandishi.

**Matokeo na Mjadala**

Sehemu hii inadadavua utata uliopo katika viambishio tamati ishilizi, mjadaala, pamoja na mapendekezo ya uchambuzi mpya wa viambishi hivyo.

***Viambishi Tamati Ishilizi (a, e, i na u) katika Vitenzi vya Kiswahili***

Vitenzi karibu vyote vya Kiswahili vina viambishi tamati ishilizi ambavyo mara nyingi ni irabu.
Irabu hizo ni *a, e, i* na *u* kama inavyoonekana katika mfano wa 1.

1. a) Analima (a-na-lim-a)
   a- kiambishi awali cha mtenda, nafasi ya tatu umoja, ngeli ya kwanza
   na – kiambishi awali cha njeo (wakati uliopo)
   lim – mzizi wa kitenzi
   *a – kiambishi tamati ishilizi*

   b) usiende (u-si-end-e)
   u- kiambishi awali cha mtenda, nafsi ya pili umoja, ngeli ya kwanza
   si – kiambishi awali cha ukanushi
   end – mzizi wa kitenzi
   *e – kiambishi tamati ishilizi*. Pia, wanaisimu wengine kama vile Mgullu (1999) hudai vilevile kinonesha dhamira amrishi

c. thubutu (thubut-u)
thubut – mzizi wa kitenzi
*u – kiambishi tamati ishilizi*

d) siendi (si-end-i)
si –kiambishi awali cha ukanushi
end- mzizi wa kitenzi
*i – kiambishi tamati ishilizi*. Wanaisimu wengi kama Ashton (1944) wanadai kinawakilisha ukanushi pia.

Katika mfano wa 1 (a-d), katika kila uchanganuzi wa kitenzi, mwishoni katika hati ya mlazo ndivyo viambishi tamati ishilizi.

Ifahamike kwamba vitenzi asilia vya Kiswahili katika mashina yake huishia na irabu *a* kabla ya kufanyiwa mabadiliko mbalimbali ya kimofolojia. Mfano lima (lim-***a***), cheza (chez-***a***), pika (pik-***a***), n.k. Pia, vitenzi vingi ambavyo si vya Kiswahili asilia, yaani vya mkopo huishia na irabu nyingine tofauti na *a*. Mfano sali (sal-i), shukuru (shukur-u), tubu (tub-u), jaribu (jarib-u) n.k. Kumekuwa na mitazamo mbalimbali juu ya dhima za irabu tamati ishilizi katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu. Mfano, Bresnan & Mchombo (1987) na Bresnan & Kanerva (1989) waanaeleza irabu *a* ijitokezayo mwishoni mwa vitenzi vya kibantu huonesha dhamira dhahiri (*indicative mood*), huku katika lugha nyingine za Kibantu inadaiwa irabu hiyo kutokuwa na maana yoyote kama asemavyo Mutaka (1994) akichukulia mfano lugha ya Kinande (moja ya lugha za Kibantu nchini Kongo). Aidha, Mgullu (1999) anatanabaisha dhamira saba za irabu zinazojitokeza mwishoni mwa vitenzi vya Kiswahili kama ionekanavyo katika Jedwali 1.

*Jedwali 1: Dhamira za Viambishi Tamati*

| Dhamira elezi yakinishi | Dhamira elezi kanushi | Dhamira ulizi yakinishi | Dhamira ulizi kanushi | Dhamira amrishi yakinishi | Dhamira amrishi Kanushi | Dhamira ya kuomba/kusihi/kuhimiza yakinishi na kanushi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ninaimb-*a* | Siju-*i* | Unachez-*a*? | Halal-*i*? | Imb-*a* | Usiimb-*e* | Tafadhali imb-*eni* |
| Tunakul-*a* | Siimb-*i* | Unaimb-*a*? | Hajalal-*a*? | Imb-*eni* | Msiimb-*e* | Tafadhali ondok-a |
| Anapik-*a* | Sitok-*i* | Ulikul-*a*? | Haimb-*i*? | Kimbi-*a* | Usikimbi-*e* | Tafadhali msiondok-*e* |

*Chanzo: Mgullu (1999)*

Pia, Rieger (2011) alichunguza viambishi tamati vitatu tu katika lugha ya Kiswahili: *a, e* na *ni.* Rieger amebainishwa kuwa viambishi hivyo vina dhima zifuatazo:

a) *a* inaonesha dhamira dhahiri *(indicative mood*) - mfano, anakul-*a*,
b) *e* inaonesha dhamira matilaba (su*bjunctive mood*) - mfano, ukanunu-*e*
c) *ni* inaonesha dhamira amri (*imperative mood*) - mfano, funge-*ni*

Aidha, Wesana-Chomi (2013) ametoa dhima moja kuu ya irabu ishilizi katika vitenzi vya Kiswahili ambayo ni kukamilisha mofolojia ya kitenzi. Mathalani, Wesana-chomi anapingana na Ashton (1944) pamoja na wanaisimu wengine wanaodai kiambishi tamati ishilizi *i* katika vitenzi kanushi (mf siimb-*i*) kinaonesha ukanushi. Wesana-Chomi anadai kwamba umbo *i* linalojitokeza mwishoni mwa vitenzi vya Kiswahili halioneshi ukanushi bali ni moja ya alomofu za maumbo yajitokezayo mwishoni mwa vitenzi, hivyo kazi yake kubwa ni kukamilisha mofolojia ya kitenzi husika. Aidha, Wesana-Chomi

anaongezea kwamba ukanushi katika vitenzi ambavyo vina umbo la irabu *i* vimeshakuwa na kikanushi tayari mwanzoni mwa kitenzi husika ambacho ni *si* au *ha***.** Wesana-Chomi anabainisha kwamba maumbo tofautitofauti yanayojitokeza mwishoni mwa vitenzi vya Kiswahili ni alomofu za mofimu moja yenye kazi kuu ya kukamilisha mofolojia ya kitenzi husika.

Ni wazi kwamba yako mawazo kinzani kuhusu ufafanuzi wa viambishi tamati ishilizi (irabu *a, e* na *i*) katika vitenzi vya Kiswahili kama ilivyobainishwa. Ukinzani wa kiufafanuzi na kiuchanganuzi unajitokeza pia katika mjadala unaohusu maumbo *-eni/-uni-ini* na *–ni.* Mathalani, ukirejea mifano ya uchambuzi ya Mgulu (1999) [angalia Jedwali 1] na Rieger (2011) [angalia aya inayoanza baada ya Jedwali 1], utabaini kwamba wanazuoni hao wanatofautina maeneo kadhaa likiwemo suala la uchanganuzi wa kiambishi tamati katika maneno kama vile *imbeni* na *fungeni*. Kama inavyonekana, msimamo wa Mgullu wa uchanganuzi wa maneno hayo ni *imb-eni/fung-eni* wakati Rieger anaamini katika *imbe-ni/funge-ni.*

***Maumbo -eni/-uni/-ini au –ni Mwishoni mwa Vitenzi vya Kiswahili***

Kama inavyoonekana katika mfano wa 2, ni kawaida kuona uchanganuzi kama huo wa vitenzi vya

Kiswahili vya namna hiyo.

2. a. Shuk-*eni*
   b. Shukur-*uni*
   c. Ondok-*eni*
   d. Kimbi-*eni*
   e. Njo-*eni*
   f. Pig-*eni*
   g. Ham-*eni*
   *h.* Salin-*ini*

Ni dhahiri kwamba utengaji huu wa mofu unaoonekana katika mfano wa 2 (a-h) ndio unaofanywa/unaochambuliwa na wanaisimu wengi akiwemo Wesana-Chomi (2013) na Mgullu (1999). Licha ya kuwa uchanganuzi huu umetamalaki katika maandiko mengi, bado kuna changamoto inayouandama uchanganuzi huo. Kudhihrisha hili, bado kuna baadhi ya wanaisimu wachache wana namna nyingine ya kuchambua aina hiyo ya maneno. Wanaisimu hao ni Rubanza (1996) anayechanganua neno limeni kwa namna hii: *lime-ni* na Rieger (2011) anayechanganua neno fungeni kama *funge-ni*. Ina maana kwamba vitenzi vilivyochanganuliwa katika mfano wa 2 vitajitokeza katika uchanganuzi tofauti kama ukizingatiwa mtazamo wa Rubanza na Rieger kama inavyoonekana katika mfano wa 3.

3. a. Shuke-*ni*
   b. Shukuru-*ni*
   c. Ondoke-*ni*
   d. Kimbie-*ni*
   e. Njoe-*ni*
   f. Pige-*ni*
   g. Habari-*ni*
   h. Hame-*ni*
   *i.* Sali- *ni*

Mfano wa 2 na 3 unaonesha ni kwa namna gani uchanganuzi wa viambishi hivyo ulivyo na changamoto. Makala hii inapendekeza uchanguzi mpya kabisa wa maumbo hayo ambapo imezingatiwa kwamba vitenzi vyote vya Kiswahili huishia na irabu kasoro vile vyenye masuala maalumu kama inavyodadavuliwa zaidi katika sehemu mojawapo ya mbele.

***Uhakiki wa Utata wa Viambishi Tamati***

Kama ilivyokwishabainishwa katika vipengele vya awali, kuwa wanaisimu wanakinzana jinsi ya kuchanganua na kufafanua viambishi tamati katika vitenzi vya Kiswahili. Mjadala wa uhakiki wa ukinzani huo baina ya wanaisimu upo katika kategoria mbili. Kategoria ya kwanza ni uchanganuzi na ufafanuzi wa viambishi *a, e, i* na *u*. Kiambishi ishilizi *u* hakitapata mjadala zaidi kwa sababu kinajitokeza kwa uchache sana hususan katika vitenzi ambavyo sio vya Kiswahili asilia (vitenzi vya mkopo ambavyo havina asili ya Kibantu). Kategoria ya pili, ni uchanganuzi na ufafanuzi wa maumbo *-eni, -uni* na *-ini.*

*Viambishi Tamati Ishilizi* ***a, e*** *na* ***i***

Viambishi tamati ishilizi *a, e* na *i* vimeelezwa kuwa na dhima mbalimbali kama ilivyoelezwa katika Jedwali 3 linalonesha kwa ufupi dhima tofauti za viambishi hivyo kutokana na wataalamu mbalimbali.

*Jedwali 3: Dhima mbalimbali za a, e na i Mwishoni mwa Vitenzi vya Kiswahili*

| Wanaisimu | Irabu ishilizi na dhima zake | | |
|---|---|---|---|
| | a | I | e |
| Mgullu (1999) | ➢ Dhamira Elezi<br>➢ yakinishi ninaimb-*a*)<br>➢ Dhamira amrishi<br>➢ (imb-*a*)<br>➢ Dhamira ya kuomba/kusihi/kuhimiza/yakinishi na kanushi (tafadhali<br>➢ ondok-*a* ) | ➢ Dhamira elezi kanushi siju-*i*)<br>➢ Dhamira ulizi kanushi (halal-*i*?) | Dhamira amrishi Kanushi (usiimb-*e*) |
| Rieger (2011) | Dhamira dhahiri (anakul-a) | - | Dhamira matilaba (Ukanunu-*e*) |
| Wesana-Chomi (2013) | Kukamilisha mofolojia ya kitenzi | Kukamilisha mofolojia ya kitenzi | Kukamilisha mofolojia ya kitenzi |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mwandishi (2025)*

Ukichunguza dhima za viambishi hivyo tamati ishilizi katika Jedwali 3, utagundua kuwa wanaisimu hao wanatofautiana katika ufafanuzi wao. Pia, yako maswali mengi kuhusu dhima hizo za viambishi tamati ishilizi walizoziwasilisha wanaisimu hao. Mathalani, Mgullu kwa namna moja au nyingine maelezo yake ni rahisi kujengewa hoja ya walakini hasa pale anapobainisha dhima zaidi ya moja ya kiambishi tamati ishilizi kimoja *a*. Ni dhahiri kwamba ubainishaj*i* wa dhima za viambishi tamati ishilizi bado hauna maelezo yenye hoja za kushawishi kisayansi kuwa kama ni kweli dhima inayobainishwa inawakilishwa na kiambishi husika kimoja. Mfano, suala la kiambishi tamati ishilizi *a* kuonesha dhamira ulizi yakinishi (unaimb-*a*?) na dhamira amrishi (ondok-*a*, nend-*a*) ni rahisi kujengewa hoja ya kuliona jambo hilo halina mashiko kwa sababu dhima hizo hazitambulishwi na maumbo yajitokezayo mwishoni mwa kitenzi bali hutambulishwa na kiimbo cha msemaji. Mfano kitenzi "*ondoka*" chaweza kuonesha dhamira ya kunyenyekea au kuamrisha kulingana na kiimbo cha

msemaji. Hata hivyo, Mgullu hajazingatia mifano ya kiambishi tamati ishilizi *e* ambayo haina ukanushi kama ambavyo imebainishwa na Rieger (2011).

Pia, suala la kuonesha kuwa kiambishi tamati ishilizi *i* kinaonesha ukanushi katika vitenzi kanushi, swali lilonaweza kuulizwa hapo ni: mbona viko pia vitenzi ambavyo havishii na *i* (bali vinaishia na *a*) lakini ni vitenzi kanushi kama vile: *hatacheza*, *hawajaimba*, *hawauipigana*? Je, upi sasa ni utofauti wa viambishi hivyo, *a* na *i* kama vyote vina dhima ya kubainisha ukanushi?

Halikadhalika, ijapokuwa maelezo ya Rieger kuhusu dhima ya irabu ishilizi *a* yamekuwa ndiyo msingi wa waandishi wengi, bado kuna mwanya wa kuhoji kama kweli dhima ya dhamira dhahiri inawakilishwa na kiambishi hicho tu au inachangiwa na jinsi utamkaji wa kitenzi husika tangu mwanzo. Vilevile, swali lingine laweza kuwa: nini hasa maana ya dhamira dhahiri? Je, haiwezi kujidhihirisha katika vitenzi visivyo na irabu ishilizi *a?*

Vilevile, kuhusu kiambishi tamati ishilizi *i*, Wesana-Chomi (2013) anakanusha kiambishi hicho kuonesha ukanushi akidai kwamba ukanushi umeshaoneshwa na mofimu fulani awali; mfano: neno *si-tak-i*, mofu ioneshayo ukanushi ni *si* na sio *i*. Hoja hiyo ndiyo inayomfanya Wesana-chomi kuwa na hitimisho kwamba irabu hizo tamati ishilizi hufanya kazi ya kukamilisha mofolojia ya kitenzi. Wesana anashadadia hoja yake kwa kudai kwamba maumbo tofautitofuti (kama vile irabu *a, e* na *i*) yanapojitokeza mwishoni mwa vitenzi vya Kiswahili yanachukuliwa kama ni alomofu mbalimbali za mofimu moja yenye kazi ya kukamilisha mofolojia ya kitenzi.

Suala la Wesana-Chomi kuona umbo *i* lijitokezalo mwishoni mwa vitenzi kanushi vya Kiswahili halina dhima ya ukanushi ni suala ambalo ni vigumu sana kulikataa lakini sio rahisi kukubaliana nalo moja kwa moja pia.

Aidha, Lupogo (2021) alifafanua ukanushi kwa kuzingatia msingi wa hadhi ya maumbo ya ukanushi na msingi wa hali ya utokeaji wa maumbo ya ukanushi. Katika msingi wa hadhi ya maumbo ya ukanushi, alibainisha kuwepo kwa maumbo ya ukanushi wa msingi ambayo ni *ha*, $si_1$[1], $si_2$,[2] *hapana,* na *to*; na maumbo ya ukanushi tegemezi ambayo ni *ku, ja, ta,* na *i*. Na kwa upande wa msingi wa hali ya utokeaji wa maumbo ya ukanushi, alibanisha aina mbili: maumbo ya ukanushi ambishi ambayo ni *ja, ta, ku, i,* na $si_2$; na maumbo ya ukanushi huru amabyo ni *hapana,* na $si_2$.

Msimamo wa makala hii juu ya suala hili na mengine umetolewa katika moja ya vipengele vinavyofuata hususan katika kipengele kinachohusu mapendekezo ya suluhisho.

*Uchambuzi wa Viambshi Tamati **-eni/-uni/-ini** na **-ni***
Kama ilivyoelezwa hapo awali kuhusu utata wa *-eni/-uni/-ini* na *-ni*, kipengele hiki kinahusika na kufanya uhakiki wa uchanganuzi wa maumbo hayo uliofanywa kwa namna tofautitofati na wanataalamu/wanaisimu mbalimbali.

Tukianza na jinsi ilivyozoeleka na wanaismu wengi katika uchanganuzi wa maneno yenye maumbo hayo kama ilivyo katika mfano wa 2 ambapo kitenzi kama *nendeni* kinachanganuliwa kama nend-*eni*. Swali linaloweza kuulizwa hapo ni: kwa nini umbo *-eni* lote linajitokeza mwishoni mwa kitenzi ilhali ipo kanuni kwamba vitenzi vya Kiswahili huishia na irabu isipokuwa katika masuala maalumu tu

[1] Hii ni kiambishi cha ukanushi kinachojitokeza katika kitenzi kikiwa kimeambatana na viambishi vingine ndani ya neno moja; mfano: *sit*akupiga

[2] Hiki ni kipashio huru cha ukanushi ambacho husimama peke yake katika tungo kanushi; mfano: huyu *si* mwizi

kama vile vitenzi vinavyobeba viambishi vya urejeshi mwishoni mwa vitenzi husika kama ionekanavyo katika mfano wa 4.

4. a. Anayetotoka - Atorokaye
   b. Anapofikia - Afikiapo
   c. Anachokula - Akulacho
   d. Anavyokula - Akulavyo

Walakini huo unaelekezwa pia katika namna ya pili ya uchanganuzi wa maumbo hayo kama inavyodaiwa na kundi jingine la wanaisimu (angalia mfano 3) ambapo wao wanadai kwamba kitenzi kama *limeni* chapaswa kichanganuliwe kama lime-*ni*. Uchanganuzi huu unazidi kuifanya changamoto iwe kubwa zaidi. Licha ya kutotimiza suala lililokwishaelezwa kuhusu kukosekana kwa ubainishaji wa kiambishi tamati ishilizi mwishoni mwa kitenzi kinachokuwa katika umbo la irabu, bado katika uchanganuzi huo taratibu za ubainishaji wa mzizi wa kitenzi/neno haujafuatwa. Hii ni kwa sababu neno *limeni*, mzizi wake ni *lim*. Mzizi ndiyo sehemu katika kitenzi hicho ambayo haibadiliki hata kama neno hilo likinyumbuliwa kiasi gani kama mfano wa 5 unavyoonesha.

5. a) Ana*lim*a
   b) Ana*lim*iwa
   c) Ki*lim*o
   d) *Lim*iwa
   e) *Lim*ika
   f) *Lim*iana
   g) Wali*lim*iwa
   h) *Lim*ishia

Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba uchanganuzi huu pia una upungufu, na kuna kila sababu ya kupendekeza uchanganuzi stahiki kama makala hii ilivyofanya katika kipengele kinachofuata.

***Mapendekezo ya Suluhisho la Utata wa Viambishi Tamati Katika Vitenzi vya Kiswahili***

Kwa kuwa utata wa viambishi tamati umelezwa katika makundi mawili, ni vizuri hata mapendekezo ya suluhisho la utata huo ukawasilishwa katika kategoria mbili ili kuwa na urari na ushikamani mzuri. Kategoria hizo ni utata wa irabu ishilizi *a, e* na *i* na utata wa viambishi tamati

*-eni/-uni/-ini* na *-ni*.

*Pendekezo la Suluhisho la Utata wa Viambishi Tamati Ishilizi* ***a, e*** *na* ***i***

Ifahamike kwamba makala hii haina lengo la kupinga kabisa na uchanganuzi na ufafanuzi uliotolewa na wanaisimu waliotangulia kuhusu viambishi tamati ishilizi *a, e* na *i* kama ilivyobainishwa hapo awali, bali lengo ni kupanua mawanda ya mitazamo ya uchanganuzi wa viambishi hivyo. Kwanza kabisa makala inakubaliana kwa kiasi fulani na madai ya Wesana-Chomi (2013) kuhusu dhima kuu ya viambishi tamati ishilizi ambayo ni kukamilisha mofolojia ya vitenzi. Lakini sio sawa kuishia hapo tu, yafaa kutoa ufafanuzi wa kinachosababisha mabadliko ya viambishi tamati ishilizi hivyo. Ni vema kutoa majibu ya swali hili: kwa nini kunakuwa na mabadiliko ya viambishi tamati ishilizi ambapo kuna wakati kitenzi hupokea kiambishi *a*, wakati mwingine *e* na wakati mwingine *i* kama mfano wa 6 unavyoonesha?

6. a) Unakul-*a*
   *b)* Hul-*i*
   *c)* Ul-*e*
   *d)* Usil-*e*

Kinachoonekana katika mfano wa 6 ni kwamba utofauti wa viambishi tamati ishilizi vyenye kazi moja kuu kama adaivyo Wesana-chomi (2013) ya kukamilisha mofolojia ya kitenzi, unasababishwa na mabadiliko mbalimbali ya kimofolojia ndani ya kitenzi hicho hususan mabadiliko yanayofanyika katika viambishi awali katika kitenzi husika. Mathalani, kitenzi kinapokanushwa, mabadiliko ya ukanushi ambayo kimsingi hujitokeza katika viambishi awali ndiyo yanayosababisha hata viambishi tamati ishilizi vibadilike.

Tukijikita na kiambishi tamati ishilizi *i,* tukiangazia zaidi katika mfano wa 7, tunaona kuwa umbo *i* limepata sura hiyo baada ya kitenzi husika kukanushwa, na ikumbukwe kwamba ukanushi huo unafanyika mwanzoni mwa kitenzi. Hata hivyo, kiambishi tamati ishilizi *i*, hujitokeza katika vitenzi kanushi katika njeo ya wakati uliopo wa mazoea tu.

7. a) Anaiba - Haib*i*
   b) Anachora - Hachor*i*
   c) Wanakula - Hawal*i*

Lakini bado kuna vitenzi kanushi ambavyo mwishoni havina umbo *i* kama ionekanavyo katika mfano 8.

8. a) Alikula - Hakula
   b) Alivaa - Hakuvaa
   c) Wameimba – Hawajaimba
   d) Atalewa – hatalewa

Hii inatukumbusha kwamba bado kuna jambo jingine la ziada la kulitolea maelezo kuhusu sifa ya kitenzi kinachotakiwa kupokea irabu ishilizi *i.* Ukichunguza kwa makini, utaona kwamba vitenzi ambavyo viko katika wakati uliopo wa mazoea ndivyo ambavyo vikikanushwa hupokea kiambishi tamati ishilizi *i.* Vitenzi ambavyo viko katika njeo ya wakati uliopita au/na ujao hata kama vikikanushwa bado vinapokea kiambishi tamati ishilizi *a* kama inavyonekana katika mfano wa 8.

Kwa hivyo, tunaona kwamba umbo linaloonesha ukanushi wa msingi ni umbo linalojitokeza mwanzoni mwa kitenzi, ambalo ni *si* au *ha.* Ni dhahiri kusema kwamba irabu ishilizi *i* inayodhaniwa au kutajwa kuwa na dhima ya ukanushi, ni mabadiliko tu yaliyosababishwa na maumbo ya msingi (*ha* na *si*) ya ukanushi yanayojitokeza mwanzoni mwa vitenzi kanushi.

Ukiachana na umbo *i,* maumbo mengine yanayotajwa kudokeza ukanushi kwa mujibu wa Ashton (1944) na Ngonyani (2002) ni kama vile *ja,* (mf. wameimba – hawa*ja*imba) na *ku* (mf. alivaa – ha*ku*vaa). Jambo hili linaungwa mkono pia na Beaudoin-Lietz (1999) ambaye anatambua kuwapo kwa maumbo matatu tu ya ukanushi ambayo ni *si*, *ha* na *to* huku akieleza kwamba maumbo mengine kama *i*, *ku* na *ja* sio maumbo yanayobeba maana ya ukanushi peke yake bali hupata maana ya ukanushi yanapoungana na maumbo ya ukanushi ambayo ni *si* na *ha*. Maana ya Beaudoin-Lietz ya maumbo hayo (*i, ku* na *ja*) hupata maana baada ya kuungana na *si* na *ha* ni sawa na hoja iliyojengwa katika makala hii kuwa maumbo hayo hubadilika kutokana na kitenzi husika kupokea viambishi awali vya ukanushi.

Kwa hivyo, kiambishi tamati ishilizi *a* hujitokeza katika vitenzi ambavyo vipo katika namna mbalimbali. Kwanza, inajitokeza katika vitenzi ambavyo havijapokea mabadiliko yoyote ya kimofolojia, yaani vipo katika hali yake ya uyakinishi na pia vipo katika hali ya kauli halisi kama vile *anaimba, analima, tunasoma* n.k. Pili, hujitokeza katika baadhi ya vitenzi vilivyopokea mabadiliko ya

kimofolojia kama vile ukanushi katika njeo kadhaa kama vile wakati uliopita (*hakunipiga*), wakati ujao (*hatanipiga*) na wakati uliopo mtimilifu (*hajanipiga*). Tatu, hujitokeza katika vitenzi vyenye hali yakinishi kwa vile *nenda* na *kimbia*.

Kwa upande wa kiambishi tamati ishilizi *e*, hujitokeza katika vitenzi yakinishi na kanushi kama vile *ufagi-e* na *usiend-e.*

Utofauti wa mahitimisho haya yaliyofanyika katika makala hi kuhusu irabu ishilizi na yale ya wanaisimu wengine kama Mgullu (1999) na Rieger (2011) ni kwamba wao (Mgullu na Rieger) wanaona viambishi hivyo pekee ndivyo hufanya kazi ya kubainsha dhima mbalimbali katika vitenzi husika. Mathalani, wanaona *e* katika kitenzi kama usiend *-e* ndiyo pekee inayoonesha hali ya amri. Makala hii haiafikiani na jambo hilo, bali inapendekezwa kwamba viambishi tamati ishilizi hivyo hubadilika tu kutokana na mabadiliko yanayofanyika katika vitenzi hivyo hususan mwanzo mwa vitenzi vya Kiswahili. Ijapokuwa dhima yake ya msingi ya viambishi hivyo ni kukamilisha mofolojia ya kitenzi husika kama ilivyosisitizwa na Wesana-Chomi (2013), bado ujitokezaji wake unahusiana na mabadiliko yaliyofanyika katika kitenzi husika hususan kwenye viambishi awali.

Suala jingine ambalo linapawa kuzingatiwa ni kwamba, kama ilivyobainishwa katika kipingele cha awali kuwa wakati mwingine ni vigumu kubaini kwamba dhima fulani imewakilishwa na kiambishi fulani pekee kama ambavyo wanaisimu waliotangulia (mf. Mgullu & Rieger) wameonesha. Hii ni kwa sababu kwamba, wakati mwingine dhima ya kitenzi hubainishwa na kiimbo cha msemaji na sio na kiambishi tamati ishilizi peke yake.

*Pendekezo la Suluhisho la Utata wa Viambishi Tamati **-eni/-uni/-ini** na **-ni***

Moja ya vipengele vilivyopita vimeeleza upungufu wa uchanganuzi wa maumbo *-eni/-uni/-ini* na *-ni.* Sababu ya msingi iliyoelezwa ni wanaisimu hao wa mwanzo kukiuka kanuni ya kuhakikisha vitenzi vya Kiswahili vinaishia na irabu na sio na maumbo yenye muunganiko wa herufi nyingi kama *-eni*, *-uni, ini* au *-ni*. Swali la msingi linaloweza kuulizwa katika uchanganuzi huo wa zamani ni: kulikuwa na haja gani ya kutoruhusu irabu za mwisho zisimame/zitengwe peke yake na zifanye kazi ileile ya kukamilisha mofolojia ya vitenzi? Jedwali 4 linaonesha uchanganuzi wa maumbo hayo kwa mujibu wa wanaisimu wa zamani na mapendekezo mapya ya uchanganuzi katika makala hii.

*Jedwali 4: Uchanganuzi wa Zamani na Mapendekezo Mapya juu ya Maumbo -eni/-uni na -ni*

| **Mtazamo wa zamani** | **Mtazamo mpya** |
|---|---|
| Lim-***eni***/lime-***ni*** | Lim-***en-i*** |
| Fung-***eni***/funge-***ni*** | Fung-***en-i*** |
| Ondok-***eni/***ondoke-***ni*** | Ondoke-**en-i** |
| Kimbi-***eni/***kimbie-***ni*** | Kimbi-***en-i*** |
| Shukur-***uni/***shukuru-***ni*** | Shukur-***un-i*** |
| S(w)alin-***ini***/s(w)li-***ni*** | S(w)al-***in-i*** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Mwandishi (2025)*

Kinachoonekana katika mtazamo wa zamani ni kwamba wanaisimu walishindwa kugundua dhima maalumu inayodokezwa na mofu *-un-, -en-,* na *-in-* kabla ya irabu ishilizi katika vitenzi vilivyobainisha katika Jedwali 4; hivyo, wakaamua kuunganisha maumbo hayo na kuyafanya kuwa kiambishi kimoja, jambo ambalo si sahihi.

Utengaji wa mofu katika mtazamo mpya unawiana kimofolojia na utengaji wa vitenzi vioneshavyo kauli ya kutendana kama ionavyojionesha katika mfano wa 9.

***9.*** a) Wanakimbiz-***an-a***
b) Wanapig-***an-a***
c) Wanasut-***an-a***

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba waliotoa mwongozo wa mwanzo wa utengaji wa mofu katika katika vitenzi vyenye muundo wa vitenzi vilivyotolewa mfano katika makala hii kama vionekanavyo katika Jedwali 4 (upande wa mtazamo wa zamani) hawakuwa wamefanya uchunguzi wa kina. Kama ilivyobainishwa katika Jedwali 4 (upande wa mtazamo mpya), huo ndio mtazamo mpya na wenye mantiki wa utengaji wa mofu za vitenzi vyenye muundo huo.

Katika Jedwali 4 (upande wa mtazamo mpya), mofu ya pili kutoka mwisho (*-en-, -un-* na *-in-*) inadokeza dhima ya upamoja, yaani utendaji wa jambo fulani unaofanywa na watu wawili au zaidi mara moja kwa pamoja. Mfano, *thubut**uni*** ni neno linatatumika kuwajuza watu wawili au zaidi waweze kufanya jambo fulani kwa pamoja; jambo ambalo huenda wao walionesha kusitasita kutokana na ugumu wa kuliendea jambo hilo wakidhani wao hawana uwezo mkubwa. Kwa hivyo, mofu ioneshayo hali ya upamoja ni **–***un-* katika neno *thubut**uni*** na umbo *i* linaendelea kubaki kiambishi tamati ishilizi chenye dhima kuu ya kukamilisha mofolojia ya kitenzi. Halikadhalika, katika maneno kama kimbi-*en-i* na ondok-*en-i* , umbo *-en* linafanya kazi ya kudokeza dhima hiyohiyo ya upamoja na *i* ni kiambishi tamati ishilizi kikamilishacho mofolojia ya neno hilo. Vilevile, katika neno sal-*in-i, in* inarejelea pia dhana ya upamoja.

***Mazingrira ya utokeaji wa Viambishi vya Upamoja (-en-, -un-, -in-)***

Ili kubaini mazingira ya utokeaji wa viambishi tamati vya upamoja, ni vema kwanza kupanua data [3] kwa kadiri inavyowezekana kama ifuatavyo:

*Kiambishi -en-:*
Kimbieni, tokeni, limeni, amueni, leteni, pigeni, pikeni, tokeni, tafuteni, shukeni, amkeni, someni, mfufueni, rukeni, pamabaneni, salieni, na msaidieni.

*Kiambishi -un-:*
Shukuruni, tubuni, abuduni, sifuni, hesabuni, kufuruni, ratibuni, thubutuni, jibuni, salimuni, na hukumuni.

*Kiambishi -in-:*
Salini, safirini, tabirini, enzini, ketini, fikirini, aminini, tathminini, tahirini, hubirini, tahinini, kabilini, na tafakarini.

*Mazingira:*
Ukichunguza data kwa makini, utabaini kwamba kiambishi tamati *-en-* hujitokeza katika vitenzi ambavyo, kabla ya kunyumbuliwa ili kupata dhana ya upamoja, vinaishia kwa irabu “a”. Mfano: kimbieni (kimbi**a**), limeni (lim**a**), amueni (amu**a**), shukeni (shuk**a**), pigeni (pig**a**), tokeni (tok**a**), na tafuteni (tafut**a**).

Kwa upande mwingine, kiambishi tamati *-un-* hujitokeza katika vitenzi ambavyo, kabla ya kunyumbuliwa kwenye dhana ya upamoja, vinaishia na irabu “u”. Mfano: shukuruni (shukur**u**), tubuni (tub**u**), abuduni (abud**u**), hesabuni (hesab**u**), kufuruni (kufur**u**), ratibuni (ratib**u**).

[3] Data hizi zilipanuliwa kwa usaidizi wa wadau wa Kiswahili katika makundi mbalimbali ya *WhatsApp* ya Kiswahili na isimu

Pia, katika kiambishi cha upamoja *-in-* hujitokeza katika vitenzi ambavyo, kabla ya kunyumbuliwa kupata dhana ya upamoja, vinaishia na irabu "i". Mfano: salini (sal**i**), safirini (safar**i**), tabirini (tabir**i**), enzini (enz**i**), fikirini (fikir**i**), aminini (amin**i**).

**Hitimisho**

Viambishi tamati katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili vimekuwa vikielezwa katika mkanganyiko na wanaisimu mbalimbali. Licha ya wanaisimu hao kupingana kati ya mmoja na mwingine, bado hoja za mwanaisimu mmoja mmoja zina upungufu fulani; hivyo, kutoa mwanya kwa mchambuzi yeyote wa lugha kuuliza maswali mbalimbali yanayokosa majibu. Kwa ujumla, wanaisimu waliotangulia wamekuwa wanatoa dhima mbalimbali za viambishi tamati ishilizi hususani *a, e,* na *i* kana kwamba viambishi hivyo vinajitosheleza peke yake kubainisha dhima fulani. Ni dhahiri kwamba irabu hizo ishilizi hubadilika kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kimofolojia hususan mwanzoni mwa kitenzi husika. Mathalani, irabu ishilizi *i* katika vitenzi kanushi imechukua umbo hilo baada ya kitenzi husika kupokea mabadiliko ya kiukanushi yanayojitikeza mwanzoni mwa kitenzi (katika viambishi awali). Vilevile, wanaisimu hao waliotangulia wanaonekana kutozingatia nafasi kimaana ya kiimbo katika tungo za Kiswahili, badala yake dhaima zote wanazichambua katika vipashio vya tungo.

Aidha, uchanganuzi wa wanaismu waliotangulia ulikuwa ukipuuza pasi na sababu ya msingi kwa baadhi ya vitenzi kuishia na irabu kama ilivyo kanuni kwa vitenzi vingi vya lugha ya Kiswahili. Hilo linathibitishwa kwa kuwapo na maumbo kama *-en*i, *-uni* au *-ni* mwishoni mwa baadhi ya vitenzi vya Kiswahili katika vitabu mbalimbali. Makala hii sasa imelirekebisha jambo hilo ambapo imetoa uchanganuzi mpya wenye kubainisha irabu ishilizi (*i*) na umbo linalobaki (-*en*, *in* na -*un*) kueleza dhima ya upamoja.

Utafiti ujao unaweza kuangazia nafasi ya kisemantiki ya kiimbo na mkazo katika lugha ya Kiswahili. Hii itawasaidia wanazuoni kutofikiria kivipa vipashio dhima ambazo zinadhihirishwa na kiimbo na/au mkazo.

**Marejeleo**

Ashton, E. O. (1944). *Swahili Grammar (Including intonation).* Longman Group Ltd.

Beaudoin-Lietz, C. (1999). *Formatives of Tense, Aspects, Mood and Negation in the Verbal Construction in Standard Swahili.* Tasnifu ya Uzamivu. Memorial University of Newfoundland. St. John's.

Bresnan, J., & Mchombo, A. S. (1987). Topic, Pronoun and Agreement in Chichewa. *Language 63(1)*, 741-782.

Bresnan, J., & Kanerva, J. M. (1989). Locative inversion in Chichewa: a case study of factorisation in grammar. *Linguistic Inquiry*, *20(1),* 1-50.

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kihore, Y. M., Massamba, D.P.B., & Msanjila, Y.P. (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo, Dar es Salaam:* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Lupogo, I. (2021). *Uchambuzi wa Ukanushi katika Kiswahili Sanifu.* Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Ltd.

Mutaka, N. (1994). *The Lexical Tonology of Kinande.* Lincom Europa.

Ngonyani, D. (2002). The morphosyntax of negation in Kiswahili. *Afrikanistische Arbeitspapiere 68, Swahili Forum* VIII, 17-33.

Rieger, D. (2011). Swahili as a tense prominent language: proposal for a systematic grammar of tense, aspect and mood in Swahili. *Swahili Forum*, *180 (1),* 114-134.

Rubanza, Y. I. (1996), *Mofolojia ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 2)*. University Press.
Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mfolojia ya Kiswahili*. Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.